## MAPITIO YA SERA
## MPYA YA MAENDELEO YA VIJANA 2019

## 1.0 UTANGULIZI

Utafiti wa Hali halisi ya Vijana nchini wakati wa kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ulifanywa katika Mikoa 12, Dar es Salaam, Mwanza, Tabora, Kigoma, Simiyu, Mara, Dodoma, Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Pwani, Mtwara and Lindi. Utafiti ulilenga kundi la vijana wa umri wa miaka 18-35 na ulihusisha Maofisa kutoka Sekretariate ya Mikoa na Serikali za Mtaa na kutoka taasisi za vijana za kitaifa na kimataifa, taasisi za mafunzo na taasisi nyingine zinazoendesha programu mbali mbali za vijana.

Maeneo takribani 7 yalifanyiwa utafiti kupitia mahojiano (structured interview) na majadiliano katika makundi (focus group discussion).masuala yaliyohusishwa ni pamoja na:

- Uelewa na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya 2007 kwa vijana na jamii kwa ujumla
- Uhusiano wa shughuli za maendeleo ya vijana na sekta nyingine kama vile Elimu, Ajira, Afya, Kilimo, Viwanda, Madini, Utalii, Utamaduni na Michezo, Sayansi na Tekinologia na Uwezeshwaji wa Vijana
- Changamoto zinazowakabili vijana
- Athari za Sayansi na Tekinologia kwa Maendeleo ya Vijana
- Mapungufu ya Kisera (policy gap)
- Wadau wengine wanaojihusisha na masuala ya vijana kuhusishwa katika Sera Mpya ya Maendeleo ya Vijana
- Mustakabali wa baadaye wa kuboresha Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana

## 2.0 JEDWALI LA UTAFITI WA HALI HALISI NA SERA YA TAIFA YA MAENDELEO YA VIJANA YA MWAKA 2007

| NA | HOJA KWENYE HALI HALISI (SITUATIONAL ANALYSIS) | ENEO KATIKA SERA MPYA YA MAENDELEO YA VIJANA | KIFUNGU KATIKA SERA MPYA YA MAENDELEO YA VIJANA | MCHANGO WA WADAU | MAONI YA SERIKALI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kutokuwepo kwa uhusiano wa moja kwa moja na uratibu wa | Sera imezingatia umuhimu wa kuhuishwa kwa masuala ya vijana | 1.2.4 | Serikali iweke mfumo mzuri wa uratibu wa | serikali itaweka mfumo wa Uratibu |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | shughuli za maendeleo ya vijana na sekta nyingine zinazojihusisha na maendeleo ya vijana. Aidha kuhuishwa kwa masuala ya vijana katika sera na mipango ya sekta na mipango ya serikali za mitaa (local government) | (youth mainstreaming) katika sera na mipango ya sekta mbali mbali aidha kuwepo na uratibu mzuri wa masuala ya vijana kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inadhamana na masuala ya Maendeleo ya Vijana | | shughuli za vijana<br><br>Kuwepo kwa dawati la vijana katika wizara, taasisi ili kufanya shughuli za vijana kwa ufanisi zaidi | utakaowezesha ofisi kusimamia masuala ya Vijana yanayofanywa na sekta nyingine kwa kushirikiana na TAMISEMI |
| 2 | Maelekezo ya utekelezaji wa shughuli za vijana yalikuwa yakifanyika kwa mtazamo wa vijana kuwa kundi moja(hetereogonous group), hivyo ushirikishwaji wa makundi yote ya vijana ikiwa ni pamoja na vijana wanaojihusisha na ukahaba, vijana wanaotumia dawa za kulevya (key population) | Sera imezingatia makundi mbali mbali ya vijana ikiwa ni pamoja na vijana wenye ulemavu, vijana wasomi, na vijana walio katika mazingira hatarishi. Kutambulika kwa vijana kulingana na makundi na mahitaji yao na kuongeza wigo wa kuwafikia vijana wote hata wale walio pembezoni (watindiga, wahadzabe) | 1.1.1 | Makundi mbali mbali ya vijana yabainishwe kulingana na hali yake na yahudumiwe kulingana na mahitaji yao | Serikali kwa kushirikiana na Wadau itahakikisha makundi mbalimbali ya vijana yanahudumiwa kulingana na hali yao na mahitaji yao |
| 3 | Huduma rafiki za kiafya zinazomjali kijana na haki ya afya ya uzazi kwa vijana | Sera imezingatia uimarishaji katika utoaji wa huduma rafiki kwa vijana katika mahospitali na kuwashirikisha vijana kwa kuwapatia elimu ya afya ya uzazi. Kuongezeka kwa elimu ya afya ya uzazi kupitia majukwaa na mikusanyiko ya vijana aidha matumizi ya taarifa za kiafya kupitia mitandao na vyombo vya habari | 1.2.8 | Kuwepo na mkakati na ufuatiliaji ili kuhakikisha huduma rafiki zinazomjali kijana zinapatikana katika hospitali na vituo vya afya mijini na vijijini<br><br>Uwepo udhibiti ya magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza kwa vijana | Serikali itaendelea kushirikiana na wadau na sekta husika kuharakisha upatikanaji wa Huduma rafiki zinazomjali kijana katika hospitali zote mijini na vijijini aidha kuendesha elimu ya afya ya uzazi kwa vijana ikiwa ni pamoja na |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | na mitandao ya kijamii, elimu na ushauri nasaha kwa vijana kuhusu magonjwa na UKIMWI, matumizi ya dawa za kulevya na kuwepo kwa vituo vya kuwarekebisha vijana (rehabilitation and sober house) | | Suala la matumizi ya dawa za kulevya ziwekewe programu na udhibiti wa kutosha<br><br>Mafunzo ya afya y a uzazi kwa vijana yatolewe kuanzia ngazi ya familia na mashuleni | huduma za ushauri nasaha kwa vijana |
| 4 | Elimu, Mafunzo na Maendeleo ya Ujuzi | Sera imezingatia eneo hili kwa kuboresha eneo la upungufu(gap) ambapo vijana wanaomaliza shule wanahitaji kupatiwa ujuzi ili waweze kujiajiri vijana wanaomaliza elimu ya juu hawana ujuzi wa kuweza kujiajiri wamekuwa wakisoma zaidi elimu ya nadharia siyo ya vitendo. Aidha kutokuwepo kwa programu za ujasiriamali na elimu ya stadi za maisha katika mitaala ya elimu.mkazo katika sekta isiyo rasmi, kuimarishwa kwa vyuo vya Ufundi Stadi na urasimishaji wa ujuzi na mafunzo. Kazini (internship and apprehentenship). | 1.2.5 | Elimu rasmi na isiyo rasmi izingatiwe katika malezi na makuzi ya vijana aidha mitaala ya Elimu ipitiwe kuhakikisha vijana wanapatiwa elimu bora inayowawezesh a kupata maarifa na kupata ujuzi wa kujiajiri mamalizapo masomo | serikali kwa kushirikiana na sekta ya Elimu, vyuo vya Ufundi(VETA) na kuimarisha mafunzo ya ujuzi kwa vijana |
| 5 | Tafsiri ya kijana (15-35) | Sera imezingatia tafsiri ya kijana kutokana na kuwepo kwa tafsiri | 1.1 | Programu zinazowaendele za vijana kulingana na | Tafsiri ya kijana (15-35) itaendelea |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | mbali mbali kulingana na mandate ya taasisi husika, kundi la vijana wanalohudumia. Aidha tafsiri zinazotolewa na Umoja wa Mataifa na hali halisi ya vijana katika nchi yetu kulingana na utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya vijana (15-35). | | tafsiri ya kijana zizingatiwe ili kuhusisha makundi yote ya vijana aidha sheria ziangalie tafsiri ya kijana ili kuondoa mkanganyiko na athari za kijamii mfano sheria ya Ndoa 1977 | kutumika kutokana na umuhimu wa kundi hili aidha tafsiri mbali mbali zitaendelea kutumika kulingana na wigo wa utekelezaji wa sekta husika |
| 6 | Utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana | Sera imezingatia suala hili ili kuwawezesha vijana kwa kuwapa mitaji kwa ajili ya shughuli zao za kiuchumi na kijamii. Sera imeweka mazingira mazuri ya ushiriki wa vijana katika shughulli za kilimo kama eneo muhimu la kukabiiana na umaskini wa kipato na kutekeleza mkakati wa kiimo kwa vijana aidha kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na mifuko mingine kama Mfuko wa Rais Mfuko wa Taifa wa Uchumi(NEEC) na fedha za mapato ya ndani asilimia 10 zinazotengwa kwa vijana, wanawake na wenye ulemavu. | 1.2.11 | Kuwepo kwa uratibu mzuri wa mfuko inayotoa mikopo kwa vijana<br><br>Masharti ya mikopo kwa vijana kupitia mifuko na mabenki yaangaliwe ili kuhakikisha vijana wote wa mijini na vijijini wananufaika na mikopo hiyo<br><br>Vijana wasiozingatia masharti ya mikopo kwa mitazamo ya kiitikadi wachukuliwe hatua kwani wanawakosesh a vijana wengine fursa ya mikopo kuendesha shughuli zao | serikali itaendelea kuratibu mifuko mbali mbali inayosaidia vijana kupata mitaji na mifuko hiyo itakuwa na masharti nafuu |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 7 | Sayansi na Tekinologia kwa Maendeleo ya Vijana | Sera imetambua umuhimu wa vijana wa kitanzania kushiriki katika Tekinologia ya Habari na Mawasiliano. Matumizi mazuri ya Utandawazi katika kuwaweza vijana kufanya kazi kwa ufanisi na kujiletea maendeleo yao. Aidha kutumia tekinologia kama sehemu ya ajira mf. Matumizi ya Simu kama wakala na njia ya mawasiliano na kutafuta masoko.suala la ubunifu kwa vijana limezingatia kama suala mtambuka katika maeneo yote ya maendeleo ya vijana | 1.2.11 | Kuwepo udhibiti mzuri wa matumizi ya TEHEMA na matumizi ya mitandao<br><br>Vijana wabunifu wabainishwe na kuendelezwa<br><br>Sheria ya matumizi ya mtandao izingatiwe na vijana wapatiwe elimu kuhusu sheria hii | serikali itaendelea kuratibu matumizi ya TEHEMA na kuhakikisha kuwa Tekinologia ya Habari na Mawasiliano inatumika vizuri kwa ajili ya kuleta ufanisi wa shughuli za vijana na kukabiliana na athari mbaya ya mitandao |
| 8 | Ushiriki na ushirikishwaji wa vijana katika masuala ya kitaifa na kimataifa | Sera imebainisha umuhimu wa vijana kushiriki kama wadau wa maendeleo yao katika masuala yanayowahusu. Kushiriki kuwepo kwa chombo cha kuwaunganisha Vijana, kushiriki makongamano ya kitaifa, kikanda na kimataifa (EAC, SADC, AU, PYU) na utekelezaji wa masuala mtambuka kama vile mazingira, jinsia na Malengo Endelevu ya Dunia (SDG.s).<br>Ushiriki wa makundi maalum | 1.2.10<br>1.13.1 | Kuwepo kwa mfumo au chombo cha kuwashirikisha vijana katika masuala yanayowahusu na kutoa mchango wao kwa serikali<br><br>Kuwepo mfumo mzuri wa kuhakikisha vijana wanashiriki katika mikutano na mkusanyiko wa kitaifa, kikanda na kimataifa | serikali itaweka mifumo ya ushiriki na ushirikishwaji wa vijana ikiwa ni pamoja na kukamilishwa kwa uundwaji wa Baraza la Vijana Tanzania |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (walemavu,vijana walio pembezoni) yamefafanuliwa kwa undani na kuwekewa mikakati madhubuti | | | |
| 9 | Majukumu ya wadau mbali mbali wa shughuli za vijana kubainishwa katika sera ya Maendeleo ya Vijana 2019 | Sera imetambua kuwa suala la vijana ni mtambuka hivyo linahusisha wadau wotekuanzia ngazi ya familia aidha ili kutekeleza shughuli za vijana kila mdau anatakiwa kutimiza majukumu yake wakiwepo vijana wenyewe. Vijana kubadili fikra zao (change of mindset) kuona jinsi wanavyoweza kushirikiana na serikali kama wadau wa kwanza wa maendeleo yao na Taifa kwa Ujumla | Sura ya Tano (Muundo wa kitaasisi) | Wadau wa shughuli za maendeleo ya vijana wawashirikishe vijana katika programu za vijana wanazoziandaa | Sera Mpya ya Maendeleo ya Vijana 2019 imebainisha majukumu ya wadau mbali mbali wa maendeleo ya vijana na kupitia tathimini na ufuatiliaji wa programu mbali mbali za vijana masuala ya vijana yataweza kutekelezwa kwa ufanisi |

## 3.0 WITO KWA VIJANA

Sera ya Maendeleo ya Vijana ni dira katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya vijana,uwepo wa sera inayotekelezeka unahitaji ushiriki na ushirikishwaji wa vijana wote katika ngazi zote, mijini na vijijini. Maboresho ya sera mpya ya maendeleo ya vijana yameweka vipaumbele vya vijana na vile vya Taifa ili kuhakikisha changamoto mbali mbali za vijana zinapatiwa ufumbuzi kwa kushirikiana na vijana na wadau vile vile kuhusishwa kikamilifu kwa Familia. Mkakati wa utekelezaji wa sera ya maendeleo ya vijana umeanisha bayana majukumu ya kila mdau katika kufanikisha sera ya maendeleo ya vijana na muda wa utekelezaji ili kuwezesha kufikiwa kwa lengo la kuwawezesha vijana nchini katika Nyanja zote za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Wito kwa vijana wote nchini ni kuhakikisha wanao ufahamu wa kutosha kuhusu Sera ya Maendeleo ya Vijana kama dira inayoongoza maisha na maendeleo yao. Vijana kubadili fikira zao hasa mitazamo ya kujihusisha kushirikiana na serikali katika kukabiliana na

changamoto mbali mbali.katika kipindi hiki cha sayansi na tekinologia vijana wanawajibika kuchukua majukumu yao kama viongozi wa leo na kesho. Aidha, kutumia vipaji vyao na ubunifu ili kuleta mawazo mapya katika kuendeleza shughuli zao na mwelekeo na dira ya nchi kama vile Dira ya Taifa 2025, Mkakati wa kuondoa umaskini, azma ya kuwa nchi yenye uchumi wa kati na Tanzania ya Viwanda.

## MAENEO YA SERA MPYA YA MAENDELEO YA VIJANA 2019

### 1.0 TAALUMA YA MAOFISA VIJANA

Sekta ya vijana bado haina watendaji wenye taaluma ya vijana. Watendaji wengi wa shughuli za maendeleo ya vijana Mkoani na Wilayani hawana taaluma ya vijana hivyo kutumia watendaji wenye taaluma ya Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii au taaluma nyingine zilizopo katika eneo husika. Kutokana na hali hii vijana wameshindwa kufaidika kitaalamu katika kushughulikia changamoto zao na masuala mengine yanayowakabili. Hivyo watumishi wenye taaluma ya vijana wanahitajika ili kuweza kutekeleza hoja zilizopo kwenye mfumo wa kisheria wa kushughulikia masuala ya vijana, kuangalia masuala ya ufuatiliaji na viwango, Takwimu za watendaji wa vijana wenye taaluma na taasisi zinazotoa taaluma hiyo. Ni kutokana na hali hii suala hili linapewa umuhimu mkubwa katika mapitio ya sera hii, taaluma hii inahitaji kutambulika kwani kama fani nyingine inatoa weledi katika kushughulikia vijana katika maendeleo yao kwa ujumla kwa kutumia mbinu mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha vijana wenyewe na wadau wa maendeleo ya vijana.

### 2.0 UZALENDO, UTAIFA NA KUJITOLEA

Utaifa, Uzalendo na Kujitolea ni muhimu katika maendeleo ya nchi.Uzalendo ni msingi mkubwa wa kujenga utaifa na kujitolea. Kujitolea ni nyenzo ya kuendeleza uraia, kuleta umoja na kutoa fursa za uendelezaji wa ujuzi miongoni mwa vijana, ipo haja ya kufanya dhana ya kujitolea kuwa na mazingira mazuri na kukuza uzalendo. Masuala haya yanaweza kufanyika kwa vijana kupitia program za malezi na makuzi.

### 3.0 HAKI NA WAJIBU WA VIJANA

vijana wanao wajibu kwa familia zao na jamii, wao ndio wahusika wakuu katika maendeleo yao na Taifa kwa ujumla. Hivyo wanatarajiwa kuweka nguvu zao na uwezo wao wote katika kulinda demokrasia, utawala wa sheria na haki za binadamu na misingi ya uhuru wetu. Vile vile vijana wanatakiwa kuhamasisha, kulinda na kuthamini utamaduni ya jamii na kumbukumbu zote za kihistoria ili waweze kurithisha kwa vizazi vijavyo.wajibu wa vijana upo pia katika kuwathamini wazazi au walezi, wakubwa na kuwasaidia kila wanapohitaji msaada kwa kuangalia amali za jamii na nchi na kulinda maisha na mshikamano ndani ya familia. Zaidi ya haya, vijana wanatakiwa kufanya kazi katika mazingira ambayo hayajaharibiwa na vitendo ya matumizi ya dawa za kulevya, ukatili na unyanyasaji wa kijinsia, vurugu za kijamii, uhalifu, unyonyaji, ubaguzi, na kuhamasisha uvumilivu,

majadiliano, ushauri na nidhamu bila kujali umri, rangi, jinsi, uwezo, dini, uraia, hali ya kijamii na kiuchumi, utaifa au masuala ya kisiasa.

## 4.0 UHUISHWAJI WA URATIBU WA MASUALA YA VIJANA

Kuhuisha masuala ya vijana katika sera zote, mikakati na program na mipango yote ndiyo mbinu itakayosaidia kuziba mapengo yanayosababisha vijana kutoshiriki katika shughuli za kijamii na kiuchumi, kitamaduni na maendeleo ya kisiasa. Mkakati wa utekelezaji wa sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana, unatambua umuhimu wa suala la idadi ya watu na vijana na haja ya kuingiza mikakati ya vijana katika ngazi zote katika mfumo mzima wa maendeleo. Uhuishaji wa masuala ya vijana unahusisha uingizwaji wa hoja za vijana wakati wa kubuni, kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathimini sera na program katika Nyanja zote za kisiasa, kiuchumi na kijamii ili vijana waweze kufaidika sawa sawa na makundi mengine katika jamii.Kuhuisha masuala ya vijana kunahitaji uratibu wenye ufanisi kwa sera zote za kisekta, mikakati, na progrmu kuhakikisha kuna utekelezaji, ufuatiliaji na tathimini ya masuala yote muhimu kwa vijana.

## 5.0 ELIMU MAFUNZO YA MAAENDELEO YA UJUZI KWA VIJANA NA KUJIAJIRIKA

Elimu na mafunzo na ujuzi ambao hauendeani na mahitaji ya soko la ajira inaendelea kuwa changamoto kubwa ya kuajirika kwa vijana. Kuajirika kwa vijana kuna lenga mambo makubwa matatu: kwanza ni kuwawezesha vijana kwa kuwapa elimu bora kulingana na mahitaji ya soko la ajira; pili kuwapa vijana elimu sahihi itakayowawezesha kujitegemea; tatu ni kuwawezesha vijana kwa kuwaandalia na kutoa ujuzi wa ujasiriamlai ambao utawasaidia kutoa ajira kwa vijana wengine. Hivyo mafunzo ya ufundi na ujuzi ni muhimu kwa maendeleo ya vijana.hata hivyo katika hali halisi ya utekelezaji wa sera ilionyesha kuwa utafiti katika suala la mahitaji ya ujuzi limekuwa Zaidi likitekelezwa kwenye sekta rasmi kuliko sekta isiyo rasmi ambayo kwa hivi sasa ndiyo mwajiri mkubwa wa vijana Pamoja na suala la ukosefu wa ajira, ni umuhimu wa kuwawezesha vijana kiuchumi. ni ukweli kuwa pamoja na hali ya kutokuwa na ajira, vijana ndiyo nguvu kazi inayohitajika katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi, katika biashara, mashamba, wajasiriamali au waajiriwa au kazi za majumbani.

## 6.0 UJASIRIAMALI KWA VIJANA NA UWEZESHWAJI KIUCHUMI

Sekta ya uchumi imepanuka kwa kiasi kikubwa. Kuimarika kwa Sekta ya gesi na mafuta ni ishara ya kuongezeka kwa fursa za ajira kwa vijana na kufungua milango ya kibiashara,

soko huria na kupanuka kwa shughuli za sekta binafsi na kilimo.katika serikali ya awamu ya tano imejidhatiti katika suala la viwanda. Maendeleo ya mijini yameongezeka na hivi sasa tunashuhudia ajira katika maeneo mengine kama vile biashara ya "bodaboda". Shughuli za ujasiriamali zimeongezeka na vijana wengine wanajishughulisha katika biashara ndogo ndogo ambazo zinawawezesha kupata kipato na hivyo kuwa mojawapo ya chanzo cha ajira. Hivyo maoni katika eneo hili yatawezesha kukuza dhana ya ujasiriamali kwa vijana na ari ya kufanya kazi na kuzingatia kauli ya Hapa ni Kazi na kukuza pato na uchumi wa vijana na Taifa kwa ujumla.

## 7.0 UBUNIFU SANAA NA MICHEZO KWA VIJANA

Mkataba wa Vijana wa Afrika unahamasisha umuhimu wa vijana kuwa wabunifu kwa ajili ya maendeleo na maisha yao kwa ujumla. Vijana wana haki ya kupumzika na kufurahia na kushiriki katika shughuli za kujiburudisha ambazo ni sehemu ya mazoezi ya afya za miili yao na kushiriki katika michezo, elimu ya mwili, maigizo, Sanaa, muziki na shughuli nyingine za kiutamaduni. Katika hoja ya uchumi wenye ubunifu suala la utamaduni na viwanda vya ubunifu ni la muhimu ikihusisha pia Sanaa, utamaduni, biashara na tekinologia. Mkakati wa kuhamasisha viwanda vya ubunifu umeanishwa katika mkakati wa utekelezaji wa sera. Kwa hii sasa sekta ya utalii inakua kwa kasi na vijana wengi wanajikita katika shughuli mbali mbali zinazohusiana na sekta hii. Kiwanda cha ubunifu kinatoa fursa ya kibiashara kupanuka duniani na kukuza uchumi. Hivyo kiwanda cha ubuniuf kinawezesha kuwa na uchumi wenye uwiano katika mzunguko wa fedha kulingana na mnyororo wa thamani ambao unatokana na shughuli zinazofanyika katika sekta hii.suala kubwa la kuzingatiwa katika kiwanda cha ubunifu ni ujuzi ambao unahitajika katika kufanikisha shughuli za sekta hii. Kiwanda ambacho mara nyingine huitwa biashara ya maonesho ni mojawapo ya sehemu inayokuza uchumi wa nchi na inahusisha mashirika mengi yanayotoa burudani.tafsiri ya sekta hii inaonyesha shughuli zinazohusisha Sanaa ya maonesho hususani muziki, sinema, luninga, redio, katuni, internet,na burudani nyingine za kiutamaduni.

## 8.0 AFYA NA USTAWI WA VIJANA

Vijana wanakabiliwa na changamoto za kiafya, ambazo husababisha kushindwa kushiriki katika elimu na sekta ya uzalishaji; changamoto hizo ni pamoja na magonjwa ya malaria, utapiamlo, UKIMWI, Magonjwa ya Ngono, dawa za kulevya na kutopata huduma rafiki za kiafya. Mtazamo wa kidunia wa changamoto za vijana upo katika upatikanaji wa ajira na magonjwa ya UKIMWI. Ingawa mwelekeo upo katika kuangalia kiwango cha maambukizi

ya UKIMWI bado kundi kubwa linaloathirika ni vijana. Suala la Dawa za kulevya miongoni mwa vijana limeendelea kuwa kubwa duniani.

Chanzo cha changamoto za kiafya kwa vijana kinahusishwa pia na masuala ya kimwili, kiakili na afya ya uzazi, hii ni pamoja na; kuongezeka kwa magonjwa ya ngono, UKIMWI, utapiamlo ambao unasababisha upungufu wa damu, uzito mdogo wa watoto wanaozaliwa na matumizi ya dawa za kulevya ambayo husababisha magonjwa ya akili, ukeketaji wa wasichana, vijana na kike na watoto; ndogo za utotoni na mimba; matumizi mabaya ya muda wa mapumziko, michezo, ukosefu wa huduma rafiki za kiafya kwa vijana na ukosefu wa taarifa sahihi hasa katika maeneo ya vijijini.

## 9.0 USHIRIKI WA VIJANA NA UONGOZI

Suala la vijana kushiriki katika Kufanya maamuzi na uongozi ni mojawapo ya mkakati uliondaliwa katika sera hii. Inatambulika kuwa vijana ndiyo wenye nguvu, wazalishaji na wakati mwingine wenye ubunifu na afya aidha ni kundi kubwa katika jamii. Ili kuhakikisha kuwa masuala yanayowakabili vijana kwa ujumla na makundi maalum ya vijana yanashughulikiwa, ni muhimu kuwa na mkakati wa kuwashirikisha vijana katika mchakato wa maamuzi na majukumu ya uongozi.hapo awali Tanzania ilikuwa na mfumo na taasisi iliyokuwa ikitumika kuwaandaa vijana katika nafasi za uongozi, mfumo huu baadaye uliondolewa, kutokana na pengo hili ipo haja kwa hivi sasa kuwa na mkakati wa kuwaandaa vijana katika uongozi. Suala hili linahitaji program maalum kuweza kutoa mafunzo ya ufahamu wa masuala ya uongozi, sifa za kiongozi, mtazamo na maadili ya vijana..

## 10.0 VIJANA NA KILIMO

Kilimo ni sekta muhimu katika maendeleo ya nchi, vijana hawana budi kushiriki kikamilifu. Serikali inatilia mkazo suala la kilimo na kuweka mazingira rafiki ya kuwawezesha vijana ikiwa ni pamoja na kuweka Mkakati wa Sera ya Kilimo kwa ajili ya vijana na wadau wengine. Kutengwa kwa maeno katika kila Halmashauri kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya vijana na kutoa mikopo nafuu kwa ajili ya kuwapa vijana mitaji ya kuendeleza miradi yao na kushiriki katia uzalishaji wa malighafi kwa ajili ya kufikia malengo ya Tanzania ya Viwanda.

## 11.0 VIJANA NA TEKINOLOGIA YA HABARI NA MAWASILIANO

TEHAMA inaweza kuwa na fursa kubwa ya kutoa elimu rasmi na isiyo rasmi, hivyo katika TEHAMA na vyombo vingine vya habari vina mchango mkubwa katika maisha ya mwanadamu na vijana kwa ujumla.vile vile TEHAMA imewezesha kuimarisha sekta ya umma na sekta binafsi, hii inajionyesha katika huduma za kiafya, elimu na huduma nyingine za mfumo wa mawasiliano katika serikali. matumizi ya tekinologia katika maisha ya vijana

shuleni imeleta manufaa kama vile mawasiliano mazuri na kuboresha shughuli zao, kumekuwepo na matumizi mabaya ya mitandao ambayo yamesababisha majeraha na maafa mengine kwa vijana. Baadhi ya mawasiliano katika mitandao hutoa mwelekeo mbaya kwa vijana.

**12.0 MASUALA MTAMBUKA KWA VIJANA**

Ni muhimu kuandaa mazingira mazuri ya mahusiano ya jinsia katika jamii kama njia ya kuthamini utu na thamani ya binadamu. Usawa wa jinsia na uwezeshwaji wa vijana unahusisha pia vijana wenye ulemavu kama chanzo cha mahusianao mazuri katika jamii na maendeleo ya kiuchumi.Vijana wanaweza na wanatakiwa kuchukua jukumu la kulinda mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Matumizi rafiki ya mazingira na mazingira ya uchumi endelevu yataboresha maisha ya mwanadamu. Dhana ya Maendeleo endelevu imekuwa suala muhimu katika program za asasi za vijana ulimwenguni kote. Kila jamii inao wajibu wa kulinda mazingira, vijana wana jukumu maalum katika kulinda mazingira kwa sababu wao ndio warithi wa mazingira hayo. Ushiriki wa vikundi vya vijana katika kukusanya takwimu za mazingira na katika kufahamu mfumo wa hali ya mazingira ni jambo la kutilia msisitizo katika kuwapatia vijana ufahamu Zaidi wa mazingira na jinsi wanavyotakiwa kushiriki katika uangalizi wa mazingira hayo. Zaidi ya haya suala la mabadiliko ya tabia nchi lina umuhimu wa kipekee katika kuhakikisha kunakuwepo kwa maendeleo endelevu na hali bora ya maisha ya vijana.